JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

MUHTASARI WA SOMO LA SAYANSI NA TEKNOLOJIA
ELIMU YA MSINGI DARASA LA III-VII
2019

© Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, 2015

Toleo la kwanza, 2015
Toleo la pili, 2016
Toleo la Tatu, 2019

ISBN 978-9987-09-058-7

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P 35094
Dar es Salaam

Simu: +255 22 2773005/+255 22 277 1358
Nukushi: +255 22 2774420
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Taasisi ya Elimu Tanzania. (2015). Muhtasari wa Somo la Sayansi na Teknolojia Elimu ya Msingi Darasa la III-VII. Dar es Salaam: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha wala kufasiri andiko hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi ya Kamishna wa Elimu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

YALIYOMO

Dibaji iv
Orodha ya majedwali v
1. Utangulizi 1
2. Uhusiano kati ya Muhtasari huu na Mtaala wa Elimu ya Msingi 1
3. Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la III-VII 1
3.1 Umahiri wa Elimu ya Msingi katika Darasa la III-VII 2
3.2 Malengo ya Somo la Sayansi na Teknolojia 3
3.3 Umahiri mkuu na umahiri mahususi katika Somo la Sayansi na Teknolojiaa 3
3.4 Ufundishaji na ujifunzaji wa Somo la Sayansi na Teknolojia 4
3.5 Upimaji wa ujifunzaji 4
4. Maudhui ya muhtasari 4
4.1 Umahiri mkuu 4
4.2 Umahiri mahususi 4
4.3 Shughuli za mwanafunzi 4
4.4 Vigezo vya upimaji 4
4.5 Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi..... 5
4.6 Idadi ya vipindi 5
5. Maudhui ya Darasa la III 5
6. Maudhui ya Darasa la IV 18
7. Maudhui ya Darasa la V 31
8. Maudhui ya Darasa la VI 48
9. Maudhui ya Darasa la VII 69

Dibaji

Elimu bora ni haki ya kila Mtanzania. Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia imekuwa ikiboresha Mtaala wa Elimu ya Msingi kuhakikisha kwamba elimu inayotolewa ni bora na inayomwandaa mwanafunzi kumudu maisha katika mazingira yake. Muktadha huu umeifanya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iboreshe mchakato wa kufundisha na kujifunza Somo la Sayansi na Teknolojia kwa muhtasari huu. Muhtasari wa Somo la Sayansi na Teknolojia umeandaliwa kwa kuzingatia Mtaala wa Elimu ya Msingi Darasa la I -VII wa mwaka 2015 toleo la 2019. Muhtasari huu unasisitiza kufundisha na kujifunza kunakozingatia ujenzi wa umahiri kwa mwanafunzi. Kwa kutumia muhtasari huu, mwanafunzi atajenga stadi za uchunguzi, udadisi, utumiaji wa taarifa za uchunguzi, na atakuza stadi za ubunifu na ugunduzi wa kisayansi na kiteknolojia.

Muhtasari wa Somo la Sayansi na Teknolojia una vipengele mbalimbali vinavyojumuisha umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za kutendwa na mwanafunzi, vigezo na viwango vya upimaji pamoja na idadi ya vipindi kwa kila umahiri mahususi. Vipengele hivi vitamsaidia mwalimu kutambua namna ya kufundisha na kupima utendaji wa mwanafunzi kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri. Hata hivyo, umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) unaendelea kupewa msisitizo katika Somo la Sayansi na Teknolojia.

Mwalimu anatarajiwa kutumia muhtasari huu kwa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa. Hata hivyo, anaweza kupanga utekelezaji wa muhtasari kwa kuzingatia mazingira yanayomzunguka.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inaendelea kupokea maoni ya kuboresha muhtasari huu kutoka kwa walimu na wadau wengine wa elimu. Maoni yote yapelekwe kwa Mkurugenzi Mkuu Taasisi ya Elimu Tanzania.

.....

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kaimu Kamishna wa Elimu
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Orodha ya majedwali

Jedwali Na. 1 Umahiri utakaojengwa na mwanafunzi katika Somo la Sayansi na Teknolojia..... 3

Jedwali Na. 2 Umahiri utakaojengwa na mwanafunzi katika Darasa la III..... 5

Jedwali Na. 3 Maudhui ya Darasa la III..... 6

Jedwali Na. 4 Umahiri utakaojengwa na mwanafunzi katika Darasa la IV..... 18

Jedwali Na. 5 Umahiri utakaojengwa na mwanafunzi katika Darasa la V..... 31

Jedwali Na. 6 Umahiri utakaojengwa na mwanafunzi katika Darasa la VI..... 56

Jedwali Na. 7 Umahiri utakaojengwa na mwanafunzi katika Darasa la VII..... 69

1. Utangulizi

Muhtasari wa Somo la Sayansi na Teknolojia umeandaliwa kwa kuzingatia Mtaala wa Elimu ya Msingi wa mwaka 2015, toleo la tatu 2019. Muundo wa sasa wa Somo la Sayansi na Teknolojia ulianza mwaka 2016. Katika mwaka huo, Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia ilibadilisha namna ya kufundisha somo hili. Mabadiliko yaliyojitokeza katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo hili ni pamoja na kufundisha stadi za Sayansi na Teknolojia kwa ujumla wake badala ya ufundishaji wa kimasomo kama ilivyokuwa hapo awali. Tafiti zinaonesha kuwa, kabla ya mwaka 2016 ufundishaji wa kimasomo ulisababisha wanafunzi kupata maudhui kwa vipande vipande hivyo kushindwa kujenga umahiri uliotarajiwa.

Somo la Sayanzi na Teknolojia linalenga kumjengea mwanafunzi maarifa, stadi na mwelekeo utakaomwezesha kukabiliana na mazingira yanayomzunguka katika maisha ya kila siku. Ufundishaji wa somo hili umelenga kumwezesha mwanafunzi kujenga umahiri hatua kwa hatua kulingana na darasa husika. Somo hili pia linasisitiza ubunifu katika kutambua fursa zilizopo katika mazingira yake na kuzitumia. Muhtasari huu umegawanywa katika sehemu kuu tatu ambazo ni utangulizi, maelezo ya jumla ya mtaala na maudhui ya muhutasari.

2. Uhusiano kati ya Muhtasari huu na Mtaala wa Elimu ya Msingi

Mtaala wa Elimu ya Msingi umebainisha mambo mbalimbali ikiwemo umahiri mkuu na umahiri mahususi katika kila somo kwa Darasa la III-VII. Muhtasari wa Sayansi na Teknolojia umewasilisha baadhi ya vipengele vya mtaala ambavyo ni malengo ya Elimu ya Msingi, umahiri wa Elimu ya Msingi, malengo ya Somo la Sayansi na Teknolojia, umahiri mkuu na mahususi, ufundishaji na ujifunzaji wa Somo la Sayansi na Teknolojia na upimaji wa ujifunzaji. Pamoja na vipengele hivi, muhtasari huu umechakata na kubainisha kwa kina maudhui, shughuli za kutendwa na mwanafunzi, vigezo vya upimaji, viwango vya utendaji, na idadi ya vipindi. Ufafanuzi huu utamwezesha mwalimu kuelewa na kutumia muhtasari huu kufundisha kwa ufasaha Somo la Sayansi na Teknolojia.

3. Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la III-VII

Elimu ya msingi ina madhumuni ya kuwapatia walengwa maarifa, stadi na mielekeo inayohitajika kwa maendeleo ya Watanzania. Malengo makuu ya Elimu ya Msingi ni kumwezesha mwanafunzi:

a) kukuza stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu na kuwasiliana;

b) kuifahamu, kuitumia na kuithamini lugha ya Kiswahili;
c) kufahamu misingi ya utawala wa sheria;
d) kuthamini utamaduni wa Kitanzania na wa jamii nyingine;
e) kukuza uwezo wa mwanafunzi kufikiri, kubuni, na kutatua matatizo;
f) kutambua umuhimu wa maadili, uadilifu na uwajibikaji kama misingi ya raia mwema;
g) kushiriki katika shughuli za michezo na sanaa pamoja na kuthamini kazi za kisanii;
h) kubaini na kukuza vipaji na vipawa vyake;
i) kuthamini na kupenda kufanya kazi;
j) kutambua, kuthamini na kutumia sayansi na teknolojia; na
k) kujiandaa kwa ngazi nyingine ya elimu pamoja na kujifunza kusiko na kikomo.

3.1 Umahiri wa Elimu ya Msingi Darasa la III-VII

Umahiri wa Elimu ya Msingi umejikita katika kumwandaa mwanafunzi kuwa na uwezo wa:

a) Kuwasiliana kwa ufasaha kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwa kuzungumza na kuandika;
b) kusoma kwa kujiamini na kufahamu maandishi sahili;
c) kutumia dhana na kanuni za kihisabati katika maisha ya kila siku;
d) kutumia stadi za kisayansi, kiteknolojia na kiufundi katika maisha halisi ya kila siku;
e) kutumia utamaduni wake na wa jamii nyingine;
f) kuheshimu tofauti za kiimani na kiitikadi katika jamii;
g) kushiriki katika michezo na shughuli za kisanii;
h) kujiheshimu na kuheshimu wengine;
i) kutumia misingi ya kizalendo katika maisha ya kila siku;
j) kushiriki katika kazi mbalimbali zinazoendana na umri wake;
k) kushiriki katika shughuli zinazokuza uwezo wake wa kufikiri kimantiki na kiyakinifu; na
l) kushirikiana na wengine kwa kufanya matendo yanayokubalika katika jamii.

3.2 Malengo ya Somo la Sayansi na Teknolojia

Malengo makuu ya ufundishaji wa Somo la Sayansi na Teknolojia kwa mwanafunzi wa Darasa la III-VII ni:

a) Kukuza uelewa na kutumia maarifa, stadi na kuwa na mwelekeo wa kisayansi na kiteknolojia;

b) kujenga uwezo wa kutumia kanuni za sayansi na teknolojia katika maisha ya kila siku; na

c) kukuza stadi za kutenda na kutumia vifaa mbalimbali vya teknolojia.

3.3 Umahiri mkuu na umahiri mahususi katika Somo la Sayansi na Teknolojia

Sehemu hii inabainisha umahiri utakaojengwa na mwanafunzi katika somo kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 1.

Jedwali Na. 1: Umahiri utakaojengwa na mwanafunzi katika Somo la Sayansi na Teknolojia

Umahiri Mkuu	Umahiri mahususi
1.0 Kufanya uchunguzi na ugunduzi wa kisayansi na kiteknolojia	1.1 Kuchunguza vitu vilivyopo katika mazingira 1.2 Kutambua aina anuai za nishati na matumizi yake 1.3 Kutambua nadharia za kisayansi na kiteknolojia
2.0 Kufahamu misingi ya sayansi na teknolojia	2.1 Kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) 2.2 Kumudu stadi za kisayansi 2.3 Kufanya majaribio ya kisayansi kwa usahihi
3.0 Kutunza afya na mazingira	3.1 Kufuata kanuni za usafi ili kuwa na afya na mazingira bora 3.2 Kufuata kanuni za afya ili kujenga afya bora 3.3 Kutambua mifumo mbalimbali ya mwili wa binadamu

3.4 Ufundishaji na ujifunzaji wa Somo la Sayansi na Teknolojia

Kufundisha na kujifunza Somo la Sayansi na Teknolojia kunazingatia zaidi vitendo, majaribio na uchunguzi ili kufikia umahiri uliotarajiwa katika somo. Mbinu shirikishi za kufundishia na kujifunzia zitatumika katika Somo la Sayansi na Teknolojia.

3.5 Upimaji wa ujifunzaji

Upimaji ni sehemu muhimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Upimaji ni sehemu muhimu katika tendo la kufundisha na kujifunza. Kupima kutamwezewa mwalimu kubaini kufikiwa kwa ujenzi wa umahiri uliokusudiwa. Kupima kutafanyika kwa kutumia zana za aina mbalimbali. Zana hizi zitajumuisha mitihani ya kuandika, hojaji, uchunguzi makini, maswali ya ana kwa ana, mkoba wa kazi na orodha hakiki. Upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi utahusisha upimaji endelevu na tamati, upimaji tamati utahusisha pia upimaji wa kitaifa ambao utafanyika kwa Darasa la IV na VII.

4. Maudhui ya muhtasari

Maudhui ya Muhtasari yamepangwa kwa kila darasa yakihusisha umahiri mkuu, umahiri mahususi , shughuli za mwanafunzi, vigezo vya upimaji, upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi na idadi ya vipindi kwa kila umahiri mahususi.

4.1 Umahiri mkuu

Huu ni uwezo wa kutenda jambo kwa usahihi na kwa ufanisi unaokusudiwa kwa muda fulani. Umahiri mkuu hujengwa na umahiri mahususi ambao hujengwa na mwanafunzi kwa kutenda shughuli mbalimbali.

4.2 Umahiri mahususi

Huu ni uwezo ambao hujengwa kwa kutenda kwa ufanisi shughuli mbalimbali zilizolengwa ndani ya muktadha wa umahiri mkuu.

4.3 Shughuli za mwanafunzi

Hivi ni vitendo ambavyo mwanafunzi anapaswa kuvitenda ili kufikia umahiri mahususi uliokusudiwa kwa kuzingatia uwezo na darasa husika.

4.4 Vigezo vya upimaji

Hivi ni viwango vya ufanisi wa utendaji wa mwanafunzi ili kufikia umahiri mahususi uliokusudiwa.

4.5 Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi

Huu ni upimaji wa kiwango cha ufikiwaji wa vigezo vya upimaji kwa kila shughuli iliyokusudiwa.

4.6 Idadi ya Vipindi

Haya ni makadirio ya muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za kutenda mwanafunzi. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika 40. Idadi ya vipindi kwa somo hili ni vipindi 5 kwa wiki. Hata hivyo, mapendekezo haya ya idadi ya vipindi yanaweza kubadilika kulingana na mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.

4.7 Maudhui ya Darasa la III

Jedwali Na. 2: Umahiri utakaojengwa na mwanafunzi katika Darasa la III

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi
1.0 Kufanya Uchunguzi na Ugunduzi wa kisayansi na kiteknolojia	1.1 Kuchunguza vitu vilivyopo katika mazingira 1.2 Kutambua aina anuai za nishati na matumizi yake 1.3 Kutambua nadharia za kisayansi na kiteknolojia
2.0 Kufahamu Misingi ya Sayansi na Teknolojia	2.1 Kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) 2.2 Kumudu stadi za kisayansi 2.3 Kufanya majaribio ya kisayansi kwa usahihi
3.0 Kutunza Afya na Mazingira	3.1 Kufuata kanuni za usafi ili kuwa na afya na mazingira bora 3.2 Kufuata kanuni za afya ili kujenga afya bora 3.3 Kutambua mifumo mbalimbali ya mwili wa binadamu

Jedwali la Na. 3 Maudhui ya Darasa la III

Umahiri Mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za mwanafunzi	Vigezo vya upimaji	Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi				Idadi ya vipindi
				Utendaji wa chini ya wastani	Utendaji wa wastani	Utendaji mzuri	Utendaji mzuri sana	
1.0 Kufanya Uchunguzi na Ugunduzi wa kisayansi na kiteknolojia	1.1 Kuchunguza vitu vilivyopo katika mazingira	a) Kubaini vitu na viumbe hai vilivyopo kwenye mazingira	Viumbe hai na vitu vilivyopo kwenye mazingira wanabainishwa kwa usahihi	Anabaini viumbe hai na vitu vilivyopo kwenye mazingira kwa kukosea	Anaweza kubaini kwa kutaja baadhi ya viumbe hai na vitu vilivyopo kwenye mazingira	Anabaini kwa kueleza viumbe hai na vitu vilivyopo kwenye mazingira na kutoa mifano	Anabaini kwa kufafanua viumbe hai na vitu vilivyopo kwenye mazingira na kuvitofautisha	21
		b) Kueleza namna ya kuchukua tahadhari za kujikinga na vitu na viumbe hatari au wenye sumu	Namna ya kuchukua tahadhari za kujikinga na viumbe hai hatari au wenye sumu zinaelezwa kwa usahihi	Anaweza kueleza namna ya kuchukua tahadhari za kujikinga na viumbe hatari au wenye sumu kwa kuchanganya	Anaweza kueleza namna ya kuchukua baadhi ya tahadhari za kujikinga na viumbe hatari au wenye sumu	Anaeleza namna ya kuchukua tahadhari za kujikinga na viumbe hatari au wenye sumu kwa ufasaha kwa kutumia mifano halisi	Anaeleza namna ya kuchukua tahadhari za kujikinga na viumbe hatari au wenye sumu na kutoa ushauri kwa wengine	
		c) Kueleza namna ya kuthamini viumbe hai na vitu katika mazingira	Namna ya kuthamini viumbe hai na vitu katika mazingira inaelezwa kwa usahihi.	Anaeleza namna ya kuthamini baadhi ya vitu na viumbe hai katika mazingira kwa kuacha vipengele muhimu	Anaweza kueleza namna ya kuthamini baadhi ya viumbe hai na vitu katika mazingira	Anaeleza namna ya kuthamini viumbe hai na vitu katika mazingira kwa ufasaha	Anaweza kueleza namna ya kuthamini vitu na viumbe hai na kutoa mifano halisi	

Umahiri Mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za mwanafunzi	Vigezo vya upimaji	Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi				Idadi ya vipindi
				Utendaji wa chini ya wastani	Utendaji wa wastani	Utendaji mzuri	Utendaji mzuri sana	
	1.2 Kutambua aina anuai za nishati na matumizi yake	a) Kueleza dhana ya nishati	Dhana ya nishati inaelezwa kwa kuzingatia vipengele vya maana, aina umuhimu kwa usahihi	Anaeleza dhana ya nishati kwa kubahatisha	Anaweza kueleza dhana ya nishati kwa kugusia baadhi ya vipengele	Anaeleza dhana ya nishati kwa maelezo fasaha	Anaweza kufafanua dhana ya nishati na kutoa mifano halisi	14
		b) Kufanya vitendo vya kuchunguza jinsi sauti, joto, na mwanga unavyosafiri	Vitendo vya kuchunguza jinsi sauti, joto na mwanga vinavyosafiri vinafanyika kwa usahihi	Anaweza kufanya vitendo vya kuchunguzia jinsi sauti, joto na mwanga vinavyosafiri bila kufuata hatua	Anaweza kufanya baadhi ya vitendo vya kuchunguzia jinsi sauti, joto na mwanga vinavyosafiri kwa kufuata hatua chache	Anafanya vitendo vya kuchunguza jinsi sauti, joto na mwanga vinavyosafiri, kwa ufanisi	Anaweza kufanya vitendo vya kuchunguza jinsi sauti, joto na mwanga unavyosafiri na kuelezea vitendo hivyo vinavyofanyika	
		c) Kueleza matumizi ya nishati ya sauti, joto na mwanga	Matumizi ya nishati ya sauti, joto na mwanga yanaelezwa kwa usahihi	Anaeleza matumizi ya nishati ya sauti, joto na mwanga kwa kubahatisha	Anaeleza baadhi ya matumizi ya nishati ya sauti, mwanga na joto na kueleweka kiasi	Anaeleza matumizi ya nishati ya sauti, mwanga na joto kwa maelezo fasaha	Anaeleza kwa kutoa mifano matumizi ya nishati ya sauti, mwanga na joto kwa usahihi	

Umahiri Mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za mwanafunzi	Vigezo vya upimaji	Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi				Idadi ya vipindi
				Utendaji wa chini ya wastani	Utendaji wa wastani	Utendaji mzuri	Utendaji mzuri sana	
	1.3 Kutambua nadharia za kisayansi na kiteknolojia	a) Kueleza dhana ya maada	Dhana ya maada inaelezwa kwa kugusia vipengele vya maana, aina na umuhimu wa maada kwa usahihi	Anaeleza dhana ya maada bila kugusia vipengele muhimu	Anaweza kueleza dhana ya maada kwa kugusia baadhi vipengele	Anaeleza dhana ya maada kwa kugusia vipengele vyote na kutoa mifano	Anaweza kufafanua dhana ya maada kwa kugusia vipengele vyote na kutoa mifano halisi	28
		b) Kufanya vitendo vya kubaini sifa za maada	Vitendo vya kubaini sifa za maada vinafanyika kwa usahihi	Anafanya vitendo na kubaini sifa za maada bila mpangilio unaostahili	Anaweza kufanya baadhi ya vitendo vya kubaini sifa za maada	Anafanya vitendo vya kubaini sifa za maada ipasavyo	Anaweza kufanya vitendo vya kubaini sifa za maada na kueleza uhusiano wa maada mbalimbali	
		c) Kutengeneza modeli/kifani kinachoweza kuelea katika maji	Modeli/Kifani kinachoweza kuelea katika maji kinatengenezwa kwa usahihi	Anatengeneza kifani/modeli kinachoweza kuelea katika maji bila kuzingatia hatua za utengenezaji	Anaweza kutengeneza modeli/kifani kwa kuzingatia baadhi ya hatua za utengenezaji	Anatengeneza kifani kinachoweza kuelea katika maji kwa ufanisi	Anaweza kutengeneza vifani vinavyoweza kuelea katika maji vya aina tofauti kwa ufanisi	

Umahiri Mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za mwanafunzi	Vigezo vya upimaji	Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi				Idadi ya vipindi
				Utendaji wa chini ya wastani	Utendaji wa wastani	Utendaji mzuri	Utendaji mzuri sana	
		d) Kutengeneza modeli/kifani kinachoweza kupaa na kuelea katika hewa	Kifani kinachoweza kupaa na kuelea katika hewa kinatengenezwa kwa usahihi	Anatengeneza kifani/modeli kinachoweza kupaa na kuelea katika hewa kwa kukosea	Anaweza kutengeneza modeli/kifani kinachoweza kupaa na kuelea katika hewa kwa kuacha baadhi ya hatua za utengenezaji	Kifani kinachoweza kupaa na kuelea katika hewa kinatengenezwa kwa ufanisi kwa kuzingatia hatua	Anaweza kutengeneza vifani/modeli vya aina mbalimbali vinavyoweza kupaa na kuelea katika hewa na kutoa mifano halisi	
2.0 Kufahamu Misingi ya Sayansi na Teknolojia	2.1 Kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)	a) Kueleza dhana ya mawasiliano	Dhana ya mawasiliano inaelezwa kwa kuzingatia vipengele vya maana, njia na umuhimu kwa usahihi	Anaeleza dhana ya mawasiliano kwa kuchanganya maelezo	Anaweza kueleza dhana ya mawasiliano kwa kugusia baadhi ya vipengele	Anaeleza dhana ya mawasiliano kwa ufasaha	Anaweza kueleza dhana ya mawasiliano na kutoa mifano halisi	21
		b) Kutumia simu	Simu inatumiwa kwa usahihi kwa kufuata maelekezo	Anatumia simu kwa kuchanganya maelekezo	Anaweza kutumia simu kwa kufuata baadhi ya maelekezo	Anatumia simu kwa kufuata maelekezo yote	Anaweza kutumia simu na kuelezea hatua za kutumia simu	

Umahiri Mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za mwanafunzi	Vigezo vya upimaji	Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi				Idadi ya vipindi
				Utendaji wa chini ya wastani	Utendaji wa wastani	Utendaji mzuri	Utendaji mzuri sana	
		c) Kueleza namna ya kutumia simu katika kujifunza	Namna ya kutumia simu katika kujifunza inaelezwa kwa usahihi	Anaeleza namna ya kutumia simu katika kujifunza kwa kuchanganya maelezo	Anaweza kuelezea baadhi ya vipengele vya namna ya kutumia simu katika kujifunza	Anaeleza namna ya kutumia simu katika kujifunza kwa mifano na ufafanuzi	Anaweza kueleza namna ya kutumia simu katika kujifunza kwa mifano na kushauri tahadhari za kuchukua	
	2.2 Kumudu stadi za kisayansi	a) Kubaini vifaa vya kurahisisha kazi	Vifaa vya kurahisisha kazi vinabainishwa kwa usahihi	Anabaini vifaa vichache vya kurahisisha kazi kwa kukosea	Anaweza kubaini baadhi ya vifaa vya kurahisisha kazi na kuvitofautisha	Anabaini na kutofautisha vifaa kwa maelezo fasaha	Anaweza kubaini vifaa vya kurahisisha kazi kwa kuvitofautisha na kuvielezea vinavyotumika	14
		b) Kufahamu vifaa vya kurahisisha kazi	Vifaa vya kurahisisha kazi vinatumiwa kwa usahihi	Anaweza kutumia vifaa vya kurahisisha kazi bila kufuata hatua za matumizi ya vifaa hivyo	Anaweza kutumia baadhi ya vifaa vya kurahisisha kazi kwa kufuata hatua chache	Anatumia vifaa vya kurahisiaha kazi kwa kufuata hatua za matumizi ya vifaa ipasavyo	Anaweza kutumia vifaa vya kurahisisha kazi na kuelezea vinavyotumika	

Umahiri Mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za mwanafunzi	Vigezo vya upimaji	Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi				Idadi ya vipindi
				Utendaji wa chini ya wastani	Utendaji wa wastani	Utendaji mzuri	Utendaji mzuri sana	
		c) Kufanya vitendo vya kutunza vifaa vya kurahisisha kazi	Vitendo vya kutunza vifaa vya kurahisisha kazi vinafanyika kwa usahihi	Anafanya vitendo vya kutunza vifaa vya kurahisisha kazi bila mpangilio wa utunzaji	Anaweza kufanya baadhi ya vitendo vya kutunza vifaa vya kurahisisha kazi	Anafanya vitendo vya kutunza vifaa vya kurahisisha kazi kwa ufanisi	Anaweza kufanya vitendo vya kutunza vifaa vya kurahisisha kazi na kueleza umuhimu wa kuvitunza	
	2.3 Kufanya majaribio ya kisayansi kwa usahihi	a) Kueleza dhana ya vipimo katika kufanya majaribio ya kisayansi	Dhana ya vipimo katika kufanya majaribio ya kisayansi inaelezwa kwa kugusia vipengele vya maana, aina na umuhimu kwa usahihi	Anaeleza dhana ya vipimo katika kufanya majaribio ya kisayansi bila kuzingatia vipengele muhimu	Anaweza kueleza dhana ya vipimo katika kufanya majaribio ya kisayansi kwa kugusia baadhi ya vipengele	Anaeleza kwa ufasaha dhana ya vipimo katika kufanya majaribio	Anaweza kueleza dhana ya vipimo na kueleza tahadhari za kuchukua wakati wa kupima	21

Umahiri Mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za mwanafunzi	Vigezo vya upimaji	Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi				Idadi ya vipindi
				Utendaji wa chini ya wastani	Utendaji wa wastani	Utendaji mzuri	Utendaji mzuri sana	
		b) Kutumia vipimo visivyo rasmi	Vipimo visivyo rasmi vinatumika kwa usahihi	Anatumia vipimo visivyo rasmi kwa kukosea	Anaweza kutumia baadhi ya vipimo visivyo rasmi	Anatumia vipimo visivyo rasmi kwa ufanisi	Anaweza kutumia vipimo visivyo rasmi na kueleza matumizi ya vipimo hivyo	
		c) Kutumia vipimo rasmi katika jaribio la kisayansi	Vipimo rasmi katika jaribio la kisayansi vinatumika kwa usahihi	Anatumia vipimo rasmi katika jaribio la kisayansi bila kufuata hatua za jaribio	Anaweza kutumia baadhi ya vipimo rasmi katika jaribio la kisayansi	Anatumia vipimo rasmi katika jaribio la kisayansi kwa kutoa mifano halisi	Anaweza kutumia vipimo rasmi katika jaribio la kisayansi na kutofautisha vipimo rasmi na visivyo rasmi	
3.0 Kutunza Afya na Mazingira	3.1 Kufuata kanuni za usafi ili kuwa na afya na mazingira bora	a) Kueleza umuhimu wa kufanya usafi wa mwili na mavazi	Umuhimu wa kufanya usafi wa mwili na mavazi unaelezwa kwa usahihi	Anaeleza umuhimu wa kufanya usafi wa mwili na mavazi kwa kuchanganya maelezo	Anaweza kueleza umuhimu wa kufanya usafi wa mwili na mavazi na kueleweka kiasi	Anaeleza umuhimu wa kufanya usafi wa mwili na mavazi kwa maelezo fasaha	Anaweza kufafanua kwa kutoa mifano ya umuhimu wa kufanya usafi wa mwili na mavazi	35

Umahiri Mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za mwanafunzi	Vigezo vya upimaji	Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi				Idadi ya vipindi
				Utendaji wa chini ya wastani	Utendaji wa wastani	Utendaji mzuri	Utendaji mzuri sana	
		b) Kutunza vifaa vya kufanyia usafi wa mwili na mavazi	Vifaa vya kufanyia usafi wa mwili na mavazi vinatunzwa kwa usahihi	Anaweza kutunza vifaa vya kufanyia usafi wa mwili na mavazi bila mpangilio unaofaa	Anaweza kutunza baadhi ya vifaa vya kufanyia usafi wa mwili na mavazi kwa kufuata mpangilio unaofaa	Anatunza vifaa vya kufanyia usafi wa mwili na mavazi kwa kufuata mpangilio unaofaa	Anaweza kutunza vifaa vya kufanyia usafi wa mwili na mavazi kwa mpangilio unaofaa na kuwashauri wengine namna ya kuvitunza	
		c) Kudumisha usafi wa mwili na unadhifu wa mavazi	Mwenendo wa kudumisha usafi na unadhifu wa mavazi unaoneshwa kwa usahihi	Anaonesha mwenendo wa kudumisha usafi wa mwili na unadhifu wa mavazi usioridhisha	Anaweza kuonesha baadhi ya matendo ya kudumisha usafi wa mwili na unadhifu wa mavazi	Anadumisha usafi wa mwili na unadhifu wa mavazi, kwa kufuata kanuni za usafi ipasavyo	Anadumisha usafi wa mwili na unadhifu wa mavazi kwa kuenzi na kuwashauri wengine waige	

Umahiri Mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za mwanafunzi	Vigezo vya upimaji	Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi				Idadi ya vipindi
				Utendaji wa chini ya wastani	**Utendaji wa wastani**	**Utendaji mzuri**	**Utendaji mzuri sana**	
		d) Kueleza dhana ya huduma ya kwanza	Dhana ya huduma ya kwanza inaelezwa kwa usahihi	Anaeleza maana ya huduma ya kwanza kwa kukosea	Anaweza kueleza dhana ya huduma ya kwanza kwa kugusia baadhi ya vipengele	Anaeleza dhana ya huduma ya kwanza kwa ufasaha na kutoa mifano halisi	Anaweza kueleza kwa kufafanua dhana ya huduma ya kwanza na kutoa ushauri kwa wenzake	
		e) Kutoa huduma ya kwanza kwa mtu aliyeumwa na wadudu hatari au wenye sumu	Huduma ya kwanza kwa mtu aliyeumwa na wadudu hatari au wenye sumu inatolewa kwa usahihi	Anaweza kutoa huduma ya kwanza kwa mtu aliyeumwa na wadudu hatari au wenye sumu bila kufuata hatua za huduma ya kwanza	Anaweza kutoa huduma ya kwanza kwa mtu aliyeumwa na wadudu hatari au wenye sumu kwa kufuata baadhi ya hatua za huduma ya kwanza	Anatoa huduma ya kwanza kwa mtu aliyeumwa na wadudu hatari au wenye sumu kwa kufuata hatua ipasavyo	Anaweza kutoa huduma ya kwanza kwa mtu aliyeumwa na wadudu hatari au wenye sumu wa aina tofauti kwa kufuata hatua za huduma ya kwanza	

Umahiri Mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za mwanafunzi	Vigezo vya upimaji	Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi				Idadi ya vipindi
				Utendaji wa chini ya wastani	Utendaji wa wastani	Utendaji mzuri	Utendaji mzuri sana	
	3.2 Kufuata kanuni za afya ili kujenga afya bora	a) Kueleza dhana ya mlo kamili	Dhana ya mlo kamili inaelezwa kwa usahihi	Anaeleza maana ya mlo kamili bila kueleweka	Anaeleza maana ya mlo kamili na kutaja baadhi ya makundi yanayounda mlo kamili	Anaeleza maana na umuhimu wa mlo kamili na kutaja makundi yanayounda mlo kamili kwa ufasaha	Anaeleza maana, umuhimu na kutaja makundi yanayounda mlo kamili kwa kutoa mifano halisi	20
		b) Kupanga vyakula vinavyounda mlo kamili	Vyakula vinavyounda mlo kamili vinapangwa kwa usahihi	Anapanga vyakula vinavyounda mlo kamili kwa kuchanganya	Anaweza kupanga baadhi ya vyakula vinavyounda mlo kamili	Anapanga mlo kamili kwa kuzingatia aina ya makundi yote ya chakula ipasavyo	Anaweza kupanga vyakula vinavyounda mlo kamili na kutoa mifano halisi	
		c) Kueleza njia za kujikinga na maambukizi ya VVU	Njia za kujikinga na maambukizi ya VVU zinaelezwa kwa usahihi	Anaeleza njia za kujikinga na maambukizi ya VVU kwa kuchanganya maelezo	Anaweza kueleza baadhi ya njia za kujikinga na maambukizi ya VVU	Anaeleza njia za kujikinga na maambukizi ya VVU kwa ufasaha	Anaweza kueleza njia za kujikinga na maambukizi ya VVU na kutoa ushauri	

Umahiri Mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za mwanafunzi	Vigezo vya upimaji	Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi				Idadi ya vipindi
				Utendaji wa chini ya wastani	Utendaji wa wastani	Utendaji mzuri	Utendaji mzuri sana	
	3.2 Kutambua mifumo mbalimbali ya mwili wa binadamu	a) Kueleza dhana ya mfumo wa mmeng'enyo wa chakula	Dhana ya mfumo wa mmeng'enyo wa chakula inaelezwa kwa kugusia vipengele vya maana na umuhimu kwa usahihi	Anaeleza maana ya mfumo wa mmeng'enyo wa chakula kwa kuchanganya maelezo	Anaweza kueleza maana na umuhimu wa mfumo wa mmeng'enyo wa chakula	Anaeleza dhana ya mfumo wa mmeng'enyo wa chakula na kutoa mifano kwa ufasaha	Anaweza kufafanua dhana ya mfumo wa mmeng'enyo wa chakula na kuhusianisha sehemu za mfumo huo	21
		b) Kuainisha sehemu za mfumo wa mmeng'enyo wa chakula	Sehemu za mfumo wa mmeng'enyo wa chakula zinaainishwa kwa usahihi	Anaainisha sehemu za mfumo wa mmeng'enyo wa chakula kwa kubahatisha	Anaweza Kutumia baadhi ya sehemu za mfumo wa mmeng'enyo wa chakula	Anaainisha sehemu za mfumo wa mmeng'enyo wa chakula kwa maelezo fasaha	Anaweza kuainisha na kutofautisha sehemu za mfumo wa mmeng'enyo wa chakula na kuelezea kazi zake	

Umahiri Mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za mwanafunzi	Vigezo vya upimaji	Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi				Idadi ya vipindi
				Utendaji wa chini ya wastani	Utendaji wa wastani	Utendaji mzuri	Utendaji mzuri sana	
		c) Kuchora mfumo wa mmeng'enyo wa chakula	Mfumo wa mmeng'enyo wa chakula unachorwa kwa usahihi	Anachora mfumo wa mmeng'enyo wa chakula bila ya kuonesha sehemu zake	Anaweza kuchora mfumo wa mmeng'enyo wa chakula na kuonesha baadhi ya sehemu zake	Anachora mfumo wa mmeng'enyo wa chakula na kuonesha sehemu zake kwa ufasaha	Anaweza kuchora mfumo wa mmeng'enyo wa chakula kwa kuonesha sehemu zake na kuzielezea	

5. Maudhui ya Darasa la IV

Jedwali la Na. 4: Umahiri Utakaojengwa na Mwanafunzi katika Darasa la IV

Umahiri Mkuu	Umahiri mahususi
1.0 Kufanya Uchunguzi na Ugunduzi wa kisayansi na kiteknolojia	1.1 Kuchunguza vitu vilivyopo katika mazingira 1.2 Kutambua aina anuai za nishati na matumizi yake 1.3 Kutambua nadharia za kisayansi na kiteknolojia
2.0 Kufahamu Misingi ya Sayansi na Teknolojia	2.1 Kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) 2.2 Kumudu Stadi za Kisayansi 2.3 Kufanya majaribio ya kisayansi kwa usahihi
3.0 Kutunza Afya na Mazingira	3.1 Kufuata kanuni za usafi ili kuwa na afya na mazingira bora 3.2 Kufuata kanuni za afya ili kujenga afya bora 3.3 Kutambua mifumo mbalimbali ya mwili wa binadamu

Jedwali la Maudhui ya Muhtasari

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za mwanafunzi	Vigezo vya upimaji	Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi				Idadi ya vipindi
				Utendaji wa chini ya wastani	Utendaji wa wastani	Utendaji mzuri	Utendaji mzuri sana	
1.0 Kufanya Uchunguzi na Ugunduzi wa kisayansi na kiteknolojia	1.1 Kuchunguza vitu vilivyopo katika mazingira	a) Kubaini vitendo vinavyo hatarisha usalama wa mazingira	Vitendo vinavyo hatarisha usalama wa mazingira vinabainishwa kwa usahihi	Anabaini vitendo vinavyo hatarisha usalama wa mazingira kwa kukosea	Anaweza kubaini kwa kutaja baadhi ya vitendo vinavyo hatarisha usalama wa mazingira	Anabaini vitendo vikuu vinavyohatarisha usalama wa kwa kutoa mifano	Anaweza kubaini kwa kufafanua vitendo vikuu vinavyohatarisha usalama wa mazingira na kushauri wengine kuacha	21
		b) Kudumisha usafi na usalama wa hewa	Usafi na usalama wa hewa unadumishwa ipasavyo	Anaonesha tabia ya kudumisha usafi na usalama wa hewa kwa kiwango kidogo sana	Anaweza kuonesha baadhi ya tabia za kudumisha usafi na usalama wa hewa	Anadumisha usafi na usalama wa hewa kwa kiwango kikubwa	Anaweza kuonyesha tabia ya kudumisha usafi na usalama wa hewa na kuwashauri wengine	

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za mwanafunzi	Vigezo vya upimaji	Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi				Idadi ya vipindi
				Utendaji wa chini ya wastani	Utendaji wa wastani	Utendaji mzuri	Utendaji mzuri sana	
		c) Kufanya majaribio ya kudhihirisha umuhimu wa mahitaji ya viumbe hai ambayo ni maji, joto, hewa, mwanga na udongo	Vitendo vya kudhihirisha umuhimu wa mahitaji ya viumbe hai vinafanyika kwa usahihi	Anafanya majaribio ya kudhihirisha umuhimu wa maji, joto, hewa, mwanga na udongo kwa kubahatisha	Anaweza kufanya baadhi ya majaribio ya kudhihirisha umuhimu wa mahitaji ya viumbe hai	Anafanya majaribio ya kudhihirisha umuhimu wa maji, hewa, joto, mwanga na udongo kwa viumbe hai kwa ufanisi	Anafanya majaribio ya kudhihirisha umuhimu wa maji, hewa, joto, mwanga na udongo kwa viumbe hai na kuhusianisha majaribio hayo	
	1.2 Kutambua aina anuai za nishati na matumizi yake	a) Kubaini vyanzo vya nishati ya umeme	Vyanzo vya nishati ya umeme vinabainishwa kwa usahihi	Anabaini vyanzo vya nishati ya umeme kwa kukosea	Anaweza kubaini kwa kutaja baadhi ya vyanzo vya nishati ya umeme	Anabaini vyanzo vikuu vya nishati ya umeme kwa maelezo fasaha	Anaweza kubaini na kufafanua vyanzo vya nishati ya umeme kwa kutoa mifano halisi	21

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za mwanafunzi	Vigezo vya upimaji	Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi				Idadi ya vipindi
				Utendaji wa chini ya wastani	Utendaji wa wastani	Utendaji mzuri	Utendaji mzuri sana	
		b) Kufanya jaribio la kubaini vitu vinavyoruhusu mwanga kupenya	Jaribio la kubaini vitu vinavyoruhusu mwanga kupenya linafanyika kwa kufuata hatua za jaribio kwa usahihi	Anafanya jaribio kubaini vitu vinavyoruhusu mwanga kupenya kwa kuchanganya hatua za jaribio la kisayansi	Anaweza kufanya jaribio la kubaini vitu vinavyoruhusu mwanga kupenya kwa kuacha baadhi ya hatua za jaribio	Anafanya jaribio la kubaini vitu vinavyoruhusu mwanga kupenya kwa kufuata hatua ipasavyo	Anaweza kufanya jaribio la kubaini vitu vinavyoruhusu mwanga kupenya kwa kufuata hatua za jaribio la kisayansi na kutoa mifano halisi	
		c) Kufanya vitendo kuonesha namna vivuli vinavyotokea	Vitendo vya kuonesha namna vivuli vinavyotokea vinafanyika kwa usahihi	Anafanya vitendo vya kuonesha namna vivuli vinavyotokea bila kuzingatia utaratibu wowote	Anaweza kufanya baadhi ya vitendo vya kuonesha namna vivuli vinavyotokea	Anafanya vitendo kuonesha namna vivuli vinavyotokea kwa kufuata maelekezo	Anaweza kufanya vitendo vya kuonesha namna vivuli vinavyotokea kwa kufuata maelekezo na kutoa mifano	

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za mwanafunzi	Vigezo vya upimaji	Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi				Idadi ya vipindi
				Utendaji wa chini ya wastani	Utendaji wa wastani	Utendaji mzuri	Utendaji mzuri sana	
	1.3 Kutambua nadharia za kisayansi na kiteknolojia	a) Kufanya jaribio la kuonesha hali tatu za maji	Jaribio la kuonesha hali tatu za maji linafanyika kwa usahihi	Anafanya jaribio la kuonesha hali tatu za maji bila kutokea mabadiliko ya hali hizo	Anaweza kufanya jaribio la kuonesha mabadiliko ya hali tatu za maji	Anafanya jaribio la kuonesha mabadiliko ya hali tatu za maji	Anaweza kufanya jaribio la kuonesha mabadiliko ya hali tatu za maji na kutoa mifano mbalimbali	21
		b) Kufanya vitendo kuonesha kizingiti cha mgando wa maji	Vitendo vya kuonesha kizingiti cha mgando wa maji vinafanyika kwa usahihi	Anafanya vitendo vya kuonesha kizingiti cha mgando wa maji kwa kukosea	Anafanya vitendo vya kuonesha kizingiti cha mgando wa maji kwa kufuata baadhi ya hatua	Anafanya vitendo vya kuonesha kizingiti cha mgando wa maji kwa kufuata hatua zinazostahili	Anaweza kufanya vitendo vya kuonesha kizingiti cha mgando wa maji kwa kufuata hatua na kutoa mifano halisi	
		c) Kufanya vitendo kuonyesha kizingiti cha mchemko wa maji	Vitendo vya kuonesha kizingiti cha mchemko wa maji vinafanyika kwa usahihi	Anafanya vitendo kuonesha kizingiti cha mchemko wa maji kwa kukosea	Anafanya vitendo vya kuonesha kizingiti cha mchemko wa maji kwa kufuata baadhi ya hatua	Anafanya vitendo kuonesha kizingiti cha mchemko wa maji kwa kufuata hatua zinazostahili	Anaweza kufanya vitendo kuonesha kizingiti cha mchemko wa maji kwa kufuata hatua na kuzielezea	

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za mwanafunzi	Vigezo vya upimaji	Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi				Idadi ya vipindi
				Utendaji wa chini ya wastani	Utendaji wa wastani	Utendaji mzuri	Utendaji mzuri sana	
2.0 Kufahamu Misingi ya Sayansi na Teknolojia	2.1 Kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)	a) Kubaini njia za mawasiliano	Njia za mawasiliano zinabaininishwa kwa usahihi	Anabaini njia za mawasiliano kwa kuchanganya maelezo	Anaweza kubaini kwa kutaja baadhi ya njia za mawasiliano	Anabaini njia muhimu za mawasiliano kwa mifano halisi ya mazingira yake	Anaweza kubaini kwa kufafanua njia za mawasiliano na kushauri wenzake kuzitumia	20
		b) Kufanya vitendo vya kutumia Redio na Luninga	Vitendo vya kutumia redio na luninga vinafanyika kwa usahihi	Anaweza kufanya vitendo vya kutumia redio na luninga kwa kuchanganya maelekezo ya matumizi	Anaweza kutumia redio na luninga kwa kufuata baadhi ya maelekezo ya matumizi	Anatumia redio na luninga kwa kufuata maelekezo ipasavyo	Anatumia redio na luninga kwa kufuata hatua za maelekezo ya matumizi na kuwaonesha wengine namna ya kutumia	
		c) Kutunza vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano mfano redio na luninga	Vifaa vya teknolojia ya habari na mawasiliano vinatunzwa kwa usahihi	Anatunza vifaa vya teknolojia ya habari na mawasiliano bila mpangilio unaofaa	Anaweza kutunza kifaa kimoja cha teknolojia ya habari na mawasiliano	Anatumia vifaa vya TEHAMA kwa kuzingatia maelekezo ya utunzaji	Anaweza kutumia vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa kuzingatia maelezo ya utumaji	

Umahiri mkuu	Umahiri mahususi	Shughuli za mwanafunzi	Vigezo vya upimaji	Upimaji wa viwango vya utendaji wa mwanafunzi				Idadi ya vipindi
				Utendaji wa chini ya wastani	Utendaji wa wastani	Utendaji mzuri	Utendaji mzuri sana	
	2.2 Kumudu stadi za kisayansi	a) Kueleza tahadhari za kuzingatia wakati wa kutumia friji na aina za majiko (jiko la mkaa, umeme, gesi, mafuta ya taa)	Tahadhari za kuzingatia wakati wa kutumia aina za majiko na friji zinaelezwa kwa usahihi	Anaelezea tahadhari za kuzingatia wakati wa kutumia aina za majiko na friji kwa kuchanganya maelezo	Anaweza kueleza baadhi ya tahadhari za kuzingatia wakati wa kutumia aina za majiko na friji	Anaeleza tahadhari za kuzingatia wakati wa kutumia aina za majiko na friji kwa maelezo fasaha	Anaweza kueleza tahadhari za kuzingatia wakati wa kutumia aina za majiko na friji na kushauri wengine namna ya kutumia	21
